

Usikawie kutafuta matibabu kwa hali ya dharura

Hujambo Minnesota, ukikabiliwa na hali ya dharura ya matibabu, piga simu kwa 911 papo hapo.

Wanaminnesota wanachukua hatua ya busara kwa kukaa nyumbani na kupunguza kasi ya kuenea kwa COVID-19.

Hata hivyo, takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya watu walio na dalili za kiharusi na mshtuko wa moyo wanaopiga simu kwa 911 au kutembelea vyumba vya dharura imepungua.

Tunataka kuhakikisha kuwa Wanaminnesota hawakawii kutafuta matibabu muhimu kwa sababu ya hofu ya COVID-19.

Mfumo wetu wa huduma za afya ni salama na umetayarishwa kutibu wagonjwa wanaopata hali yoyote ya dharura ya kimatibabu.

Ukikabiliwa na hali dharura ya matibabu, piga simu kwa 911 papo hapo.

Hii ni pamoja na kuvuja damu bila kukoma, kushindwa kupumua, kupoteza fahamu ghafla au dalili za kiharusi au mshtuko wa moyo.

Kupokea matibabu haraka inaweza kuokoa maisha yako.

Minnesota Department of Health
Communications Office
PO Box 64975
St. Paul, MN 55164-0975
651-201-4989
health.communications@state.mn.us
www.health.state.mn.us

10/27/20

Don't Delay for Medical Emergencies (Swahili)

To obtain this information in a different format, call: 651-201-4989